**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 2 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.366
*Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi katika Ujifunzaji wa Isimu: Mifano kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA)*

# Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi katika Ujifunzaji wa Isimu: Mifano kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

Sauda Uba Juma
*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2023-11-12*
*Rekebishwa: 2023-11-23*
*Kubalika: 2023-11-18*
*Chapishwa: 2023-12-19*

***Maneno Muhimu***
Makosa
Ujifunzaji
Isimu

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Juma, S. U. (2023). Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi katika Ujifunzaji wa Isimu: Mifano kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *2*(1), 17-28.

*Copyright © 2023*
BY NC SA

**Ikisiri**
Makala haya yanachunguza na kutathmini makosa yanayofanywa na wanafunzi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa kozi mbalimbali za kiisimu kwa wanafunzi MNMA. Mchakato huo uliangaza wanafunzi wanaosoma kozi za isimu ya Kiswahili darasani. Lengo la kuona haja ya uchunguzi huo, ni kubaini makosa mbalimbali yanayofanywa na wanafunzi hao na kutafuta njia mbadala ya kuweza kuwasaidia. Data za makala haya zilikusanywa kwa njia nne ambazo ni: Mosi, udurusu wa nyaraka mbalimbali maktabani ili kuwa na welewa mpana zaidi unaohusu vipengele anuwai vya kiisimu vilivyochunguzwa. Pili, hojaji ambazo zilihusisha vipengele mbalimbali vya kiismu kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki zilitumika kwa ajili ya kupata data na kubaini makosa ya kiisimu yaliyojitokeza. Tatu, usaili ambapo baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kinasibu, walitakiwa kutoa maoni yao na kujadiliana na mtafiti kuhusu vipengele hivyo. Mwisho, njia ya ushuhudiaji ilitumika wakati wa mijadala iliyoendeshwa darasani katika vipindi vyao kulingana na ratiba iliyowekwa. Njia hii ilitusaidia kupata data za kiisimu kupitia utamkaji na uzungumzaji. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba kuna matatizo kadhaa ambayo yanawakwama wanafunzi na kusababisha kufanya makosa na kuona ugumu katika kujifunza isimu ya Kiswahili. Hivyo, makosa hayo yaliyofanywa yamebainishwa na kupendekeza namna bora ya kuwasaidia vijana hao ili baadhi yao wasiendelee kuzichukia baadhi ya kozi za kiisimu kama vile fonoloji, mofoloji, sintaksia na semantiki.

## Utangulizi

Dhana ya isimu imefasiliwa na wataalamu mbalimbali wa kale na wa sasa miongoni mwao ni: Hartman (1972) ambaye anaeleza kwamba isimu ni eneo maalumu la mtalaa ambalo lengo lake huwa ni kuchunguza lugha. Wanaisimu huzichunguza lugha zikiwa ni nyenzo muhimu za mawasiliano ya mwanadamu. Naye Besha (1994) anafafanua kwamba isimu ni taaluma ambayo huchunguza na kuweka bayana kanuni ambazo ndizo msingi wa kila lugha. Kwa upande wake Massamba (2004) anasema kwamba isimu ni taaluma ya ufafanuzi, uchambuzi na uchanganuzi wa lugha kwa kutumia


17

mbinu za kisayansi. Aidha, Mdee na wenzake (2011) wanasema kwamba isimu ni taaluma ya kuchunguza sayansi ya lugha. Kwa mujibu wa fasili zilizotolewa na wataalamu hao, tunaweza kusema kwamba isimu ni taaluma inayochunguza na kuchambua lugha kwa kutumia misingi ya kisayansi. Hivyo basi, ismu ni sayansi ya matamshi, maumbo, miundo, maana na matumizi ya lugha.

Sayansi nayo imepambanuliwa kama elimu au maarifa yanayotokana na uchunguzi makinifu kuhusu kitu au tukio, wenye sifa za uyakinifu, upangilifu na uwazi (Munyua 2007). Kwa ujumla kuna mambo kedekede yanayoweza kufanyiwa uchunguzi katika lugha. Mathalani uchunguzi unaweza kufanywa kuhusu muundo wa lugha, matumizi yake kisanaa, uamilifu wake kijamii, uhusiano wake na taaluma zingine kama vile saikolojia, elimu jamii, anthropolojia na nyinginezo. Kwa msingi wa makala haya tunajiegemeza zaidi na isimu kama sayansi ya lugha, tukiangazia zaidi muundo wake. Muundo huo unajikita katika vipengele vyake vya msingi vya kiismu ambavyo ni fololojia, mofolojia, sintaksia na semantiki.

Wataalamu na wanazuoni mbalimbali wameshafanya utafiti kuhusu kuhusu makosa yanayofanywa katika vipengele mbalimbali vya kiisimu vya lugha ya Kiswahili na baadhi ya lugha za Kibantu. Miongoni mwao ni hawa wafuatao ni: Idarus (2005) alifanya utafiti kuhusu makosa yanayofanywa mara kwa mara katika matumizi ya Kiswahili. Uchunguzi wake ulifanyika katika jiji la Dar es Salaam kati ya Januari 1979 na Oktoba 1979. Mtafiti huyo aliangazia zaidi katika vyombo vikuu rasmi vya habari vinavyotumia Kiswahili. Hivyo, matokeo ya utafiti yalionesha kwamba kuna makosa mabalimbali ya kiisimu yanayofanywa katika lugha ya Kiswahili kupitia vyombo hivyo. Mathalani makosa ya msamiati, kama vile matumizi ya maneno *jambazi* (jitu katili) na *jangili (*mwindaji haramu katika mbuga za wanyama)*, nona* (linatumika kwa mnyama) na *nenepa* (linatumika kwa binadamu) pamoja na *barabara* (nja iliyotengenezwa maalumu kwa ajili ya kupita watu au magari) na *mtaa* (eneo fulani katika mji). Kwa maoni yake maneno hayo yana maana tofauti lakini baadhi ya watu wanayachanganya katika matumizi.

Mbali na kipengele cha msamiati utafiti wa Idarus ulichunguza kipengele cha kimuundo. Katika kipengele hicho alibainisha miundo kama *sijala tena na nikamkutana,* miundo hiyo kwa maoni yake haikubaliki katika Kiswahili sanifu. Badala yake miundo hiyo ilipaswa iwe *sijawahi kula* na *nikakutana naye.* Kiukweli utafiti wa Idarus pamoja na kuwa umejikita kuchunguza baadhi ya makosa ya kiismu, unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa umekita katika kuchunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi wa MNMA katika kujifunza kozi mbalimbali za kiisimu darasani. Vilevile, utafiti huu umependekeza njia ambazo zitasaidia kupunguza makosa hayo kwa wanafunzi jambo ambalo halikufanywa katika utafiti wa Idarus.

Utafiti mwingine ni ule wa Munyua (2007) ambaye alichunguza kuhusu makosa ya kisarufi yanayofanywa na walimu na wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Katika utafiti wake anaeleza kuwa maneno ya Kiswahili yanaweza kuainishwa katika makundi mbalimbali ya ngeli. Uainishaji huo kwa kawaida hutawala uwiano wa kisarufi kati ya nomino kwa upande mmoja pamoja na vitenzi na vivumishi kwa upande mwingine. Hivyo vile vionyeshi vya uwiano hutambulisha idadi na nafsi kwenye neno (kitenzi au kivumishi) vinamoambishwa. Aliendelea kudai kwamba wanafunzi wa Kiswahili ambao mifumo yao ya lugha-mama haina uainishaji wa ngeli kama wa Kiswahili, mathalani Kiluo na Kinandi wanapata shida kuambisha vionyeshi mwafaka vya uwiano wa kisarufi. Makosa ya yanayotokana na upatanishi huo ni kama yanavyojitokeza katika sentensi zifuatazo:

i. Gari anaondoka
ii. Somo hiki ni kigumu
iii. Viatu hizi ni zangu

iv Mwanafunzi ule ni mtoro

Utafiti wa Munyua umekuwa ni rejeo la msingi katika utafiti huu kwa kuwa limetusaidia kupata data zinazohusiana na makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya. Motokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba baadhi ya makosa hao yanafanana na mengine yanatofautiana na yale ya kiisimu yanayofanywa na wanafunzi wa MNMA.

Baadhi ya wanazuoni wamefanya utafiti kuhusu makosa ya kiisimu yanayofanywa na jamiilugha mbalimbali kutokana na athari za lugha zao za kwanza. Miongoni mwao ni hawa wafuatao: Otiende (2013) alifanya utafiti na kuchunguza kuathiriana kwa lugha kiisimu. Katika utafiti wake alibainisha athari za kifonolojia za Kiolusuba katika Kiswahili ambapo aligundua makosa yanayotokana na kuzichanganya sauti za lugha yao katika Kiswahili. Kwa mfaano sauti /sh/ katika Kiolusuba inakuwa /s/ katika Kiswahili, /dh/ inakuwa /s/ na /ch/ inakuwa /j/. Aidha, Athumani (2015) alichunguza athari za Kiyao katika Kiswahili na kubaini makosa ya kifonolojia katika Kiswahili yanayotokana na athari za Kiyao. Mathalani, sauti /k/ ambayo inabadilika na kuwa /ch/ na sauti /m/ inabadilika na kuwa /n/. Hata hivyo maelezo ya watafiti hao ni ya jumla mno kwa kuwa, ingekuwa muafaaka zaidi walau wangetoa mifano ya maneno ya Kiswahili yenye athari ya sauti za lugha hizo za Kibantu wanazozizungumzia.

Mbilinyi (2021) alifanya utafiti kuhusu kuathiriana kwa kipengele cha fonolojia na mofolojia katika lugha ya Kiwanji na Kiswahili. Katika utafiti wake alibainisha makosa ya kifonolojia na kimofolojia katika Kiswahili yanayotokana na athari ya Kiwanji. Makosa ya kifonolojia aliyoyabainisha ni pamoja na athari za kimadende /r/ katika Kiwanji inayotumika badala ya kitambaza /l/ katika Kiswahili. Hivyo maneno ya Kiwanji yaliyo na sauti ya kimadende /r/ wakati wa uzungumzaji, yanatumia sauti ya kitambaza /l/. Aidha, kuna kuathiriana kwa ngeli za Kiwanji na Kiswahili kwa mfano katika Kiswahili, kiambishi awali ni ngeli ya nomino husika wakati katika Kiwanji kunakuwa na kiambishi awali kinachotangulia kiambishi cha ngeli husika. Matokeo yake maneno ya Kiswahili yanayotamkwa katika Kiwanji yanaathiriwa na hali hiyo. Mathalani *wazazi, mpira na mama* katika Kiswahili, yanatamkwa *awazazi*, *upila na umama* katika Kiwanji. Utafiti wa Mbilinyi ni wa muhimu katika utafiti huu ingawa unatofautiana kwa kuwa utafiti huu, umejikita na makosa ya kiisimu yanayofanywa na wanafunzi wa MNMA katika Kiswahili. Pia kupendekeza njia ambazo zinaweza kufanyika ili kupunguza makosa ya Kiisimu kwa wanafunzi hao.

**Mwega wa Kinadharia**

Makala haya yanaongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL). Nadharia ya UL iliasisiwa na mwanaisimu Lado katika miaka ya (1950). Kazi ya kwanza ambayo ilitumia nadharia hii ilimhusu Lado mwenyewe Msingi mkuu wa nadharia hii ni kuangalia matokeo ya matumizi ya lugha mbili katika jamiilugha moja. Katika msingi huo mkuu, kuna misingi mingine midogomidogo ndani yake ambayo ni: kulinganisha athari zinazoweza kujitokeza katika lugha husika. Pia, kulinganisha na kutofautisha matokeo ya lugha mbili au zaidi zinazotumiwa katika jamiilugha moja. Vilevile, kuweza kuyatumia matokeo hayo ya kuathiriana kwa lugha mbili au zaidi kwa ajili ya maendeleo ya lugha hiyo au hizo katika jamii inayohusika. Hivyo basi, katika makala haya nadharia ya UL imetumika na kusadifu barabara kwa kuwa tumechunguza vipengele vya kifonolojia na kimofoloojia ambavyo vinasababisha ugumu kwa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa isimu ya lugha ya Kiswahili.

Tumebaini kwamba baadhi ya wanafunzi wameathiriwa na lugha mama zao kiasi ambacho wanachanganya baadhi ya vipengele hivyo vya kiiismi vya lugha yao na kuvitumia katika lugha ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, mbali na vipengele vya kifonolojia na kimofolojia, nadharia hii imetumika na kufafanua vipengele vingine vya kiisimu ambavyo ni sintaksia na semantiki. Madai haya

yalitolewa na James (1980) ambapo alibainisha vipengele hivyo alipokuwa akifafanua nadharia ya UL. Hivyo, kwa kuwa utafiti huu ulichunguza makosa wanayafanya wanafunzi katika kufundisha na kujifunza isimu ya Kiswahili, ni dhahiri kwamba, nadharia hii imetusaidia kuvibaninisha vipengele vya kiisimu vya lugha ya Kiswahili na jinsi vinavyoathiriwa na lugha nyingine za Kibantu.

**Methodolojia**

Kama ambavyo tumefafanua katika ikisiri kwamba utafiti huu ulihusisha ukusanyaji wa data katika vyanzo mbalimbali, Njia ya kwanza ilikuwa ni usomaji wa nyaraka zinazohusu isimu ya Kiswahili kwa ujumla ambapo vitabu na majarida mbalimbali yalitumika ili kuwa na uelewa mpana kuhusu mada tuliyoichunguza. Njia ya pili iliyotumika ilikuwa ni ukusanyaji wa taarifa kupitia hojaji ambazo tuliziandaa kwa ajili ya kujibu maswali mbalimbali. Hojaji hizo zilihusisha vipengele anuwai vya fonolojia, mofolojia, sintaksia pamoja na semantiki ambapo wanafunzi walitakiwa kujibu maswali hayo ili kubaini makosa yaliyoyafanya katika kujaza hojaji hizo.

Vilevile, njia ya tatu ilikuwa ni usaili ambapo mtafiti alijadiliana na wanafunzi ili kupata taarifa za kina kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi hao pamoja na ugumu wanaoupata katika kujifunza isimu ya Kiswahili darasani. Mwisho, data za utafiti huu zilikusanywa kupitia njia ya ushuhudiaji. Kwa kutumia njia hii tulihudhuria mihadhara mbalimbali ya kozi za kiisimu darasani ili kuangalia na kuona jinsi wanafunzi wanavyozungumza na kutamka maneno mbalimbali. Kama wanavyodai Msanjila na wenzake (2011), ni muhimu kuchunguza matumizi ya lugha yasiyokubalika kulingana na kanuni za lugha hii ya Kiswahili. Kwa kusikiliza mazungumzo mbalimbali tutagundua vibainishi vya lugha, vibainishi hivi vya lugha vinaweza kuwa vya kifonolojia, kimofolojia, kileksika na kisemantiki. Katika sehemu inayofuata tutaangazia makosa yanayofanywa katika kujifunza kozi za isimu ya Kiswahili kwa wanafunzi wa MNMA.

**Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kulingana na jinsi makosa mbalimbali ya kiisimu yalivyojitokeza kama ifuatavyo:

**Fonolojia**

Katika kipengele hiki tumejikita katika kuchunguza utamkaji wa sauti zinazotumika katika Kiswahili. Hii ina maana kwamba katika uwanja huu, tunavitazama vitamkwa kama sauti bainifu. Tunaposema sauti bainifu, tuna maana ya zile sauti ambazo huleta tofauti ya maana katika maneno ya Kiswahili. Tukizingatia jinsi vitamkwa hivi vinavyosikika masikioni mwetu, tutabaini kwamba utamkaji wa sauti /l/ ni tofauti na utamkaji wa sauti /r/, kadhalika utamkaji wa sauti /f/ ni tofauti na utamkaji wa sauti /v/. Sauti /l/ ambayo ni kitambaza kinachotamkiwa kwenye ufizi, baadhi ya wanafunzi walikuwa wanaichanganya na sauti ya kimadende cha ufizi /r/. Halikadhalika sauti /f/ na /v/ zote ni vikwamizi ambavyo vinatamkiwa kwenye mdomo na meno. Hata hivyo, sauti /f/ inatoka katika kinywa kwa mguno hafifu wakati sauti /v/ inatoka kwa mguno wa nguvu.

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani sauti hizo zilikuwa na athari kubwa katika isimu ya Kiswahili. Kupitia mbinu ya ushuhudiaji tulibaini kuwa baadhi ya wanafunzi walikuwa wanafanya makosa ya kuzichanganya katika utamkaji. Pia njia ya ushuhudiaji pamoja na hojaji zilizojazwa zilionesha makosa ya kiuandishi wa baadhi maneno ya Kiswahili. Kwa mfano badala ya kutamka au kuandika maneno kama *kalamu, kura, viatu, thamani, mtu* n.k. Maneno hayo yalitamkwa *karamu, kula, fiatu, samani*, na *ntu*. Tatizo la kuzichanganya sauti hizo linaweza kuonekana ni la kawaida katika uzungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Tunaseama hivyo, kwa sababu tunapozungumza tunaelewana katika mawasiliano ya kawaida ya kila siku. Vilevile, katika lugha ya

mazungumzo, athari kama hizo wakati mwingine zinavumilika kwa kuwa lugha ya mazungumzuo inaweza kukiuka kaida zake muradi lengo la mawasiliano lifikiwe.

Hii ni kinyume, na matumizi ya lugha sanifu kama ambayo tunaitumia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Ni dhahiri kwamba ubadilishaji huo wa sauti una athari kubwa ambazo haziwezi kuvumilika katika isimu ya Kiswahili. Tukichunguza maneno hayo tuliyoyabainisha, tutagundua kwamba kutumia neno *kalamu* badala ya *karamu* kwa mfano au *kula* badala ya *kura* ni upotoshaji mkubwa katika lugha ya Kiswahili. Maneno yote hayo ingawa yanaonekana kukaribiana katika utamkaji, yana maana tofauti ambazo hazina uhusinao wowote katika lugha ya Kiswahili.

Tukiachilia mbali kipengele hicho cha kubadilisha sauti katika utamkaji na uandishi wa maneno ya Kiswahili, baadhi ya wanafunzi wanaojifunza kozi mbalimbali za isimu ya Kiswahili pia, wanafanya makosa ya udondoshaji wa sauti /h/ katika baadhi ya maneno yenye sauti hiyo. Kwa mfano, neno *haimo, hana, hiari, hina, hula* n.k. yanatamkwa *aimo, ana, iari, ina* na *ula*. Udondoshaji wa sauti /h/ huleta maana tofauti katika Kiswahili. Kwa mfano John *ana* kosa badala ya John *hana* kosa au yeye *atafika* badala ya yeye *hatafika*.

Sambamba na makosa ya udondoshaji, kuna makosa mengine yanayofanywa na wanafunzi wa MNMA wanaosoma kozi za isimu ya Kiswahili. Baadhi ya wanafunzi chuoni hapo wanashindwa kutofautisha sauti zenye mpumuo[1] na zile ambazo hazina. Mathalani sauti /č$^h$/, /k$^h$/, /p$^h$/ na /t$^h$/ katika maneno *ch$^h$anga* (isiyokomaa), *k$^h$amba* (aina ya samaki wa baharini) *p$^h$aa* (aina ya mnyama wa porini) na *t$^h$aa* (samaki) kimtawalia. Sauti za mpumuo zinatofautiana na sauti zisizo na mpumo ambazo ni /č/, /k/, /p/ na /t/ katika maneno *changa,* (dunduliza kitu kidogokidogo ili kiwe kingi) *kata,* (kifaa kinachotumika kunywea maji) *paa* (sehemu ya juu ya nyumba) na *taa* (kifaaa kinachowashwa na kutoa mwangaza kwa ajili ya kuonea). Katika Kiswahili sauti za mpumuo hazijidhihirishi waziwazi kama mojawapo ya sifa bainifu ya sauti kiotografia (Juma 2019). Hata hivyo kimatamshi, sauti hizo zinajidhihirisha kwa kuwa zinabadilisha maana za maneno. Sababu ya kutojitokeza mpumo katika uandishi, inaelezwa kuwa inatokana na matatizo ya usanifishaji wa lugha hii uliofanywa na wageni tangu kipindi cha ukoloni kama asemavyo Mbaabu (2007):

> *Tumesanifisha Kiswahili na katika kufanya hivyo yaonekana Kiswahili kimekuwa lugha mpya. Kiswahili kitaendelea kupanuka katika nyanja mbalimbali lakini maendeleo hayo inafaa yatokane na mawazo ya Waswahili; haifai kuwalazimisha kuyapokea. Lakini tuko katika harakati za kuwafunza Waswahili lugha yao kupitia vitabu ambavyo si vya Kiswahili. Hatimaye tumepata mwana haramu huyu Kiswahili cha Kiingereza*…uk. 38-39.

Vilevile, utafiti huu ulibaini kwamba baadhi ya wanafunzi, wanashindwa kuzitofautisha sauti zenye athari za kigeni kutoka katika lugha ya Kiarabu. Sauti kama /θ/, /ð/ na /ɣ/ katika maneno *thawabu* (matendo mema anayolipwa mja na Mola wake), *dhahabu* (aina fulani ya madini) na *ghali* (kitu chenye bei ya juu). Sauti hizo zenye asili ya lugha ya Kiarabu zinatofautiana kimatamshi na kimaana na zile ambazo hazina asili ya lugha ya Kiarabu kama vile /s/, /z/ na /h/. Mathalani, maneno *sawabu* na *zahabu* yanatamkwa na baadhi ya wanafunzi kimakosa kinyume na taratibu za isimu ya lugha ya Kiswahili. Halikadhalika, neno *hali/gali* lina maana tofauti na neno na *ghali* ambapo tofauti hizo zinasababishwa na matumizi ya sauti /h/ na /ɣ/. Aidha, neno *samani* maana yake ni vitu vya kuchonga vinavyotengenezwa na fundi seremala kama vile makabati, meza, vitanda na vinginevyo wakati neno *thamani* maana yake ni gharama au ubora wa kitu kwa mujibu wa kitu chenyewe (Kamusi

[1] Utamkaji wa sauti k.v k, p, au t kwa kuachia viungo vya sauti hizo kwa nguvu (BAKIZA,2010: 267)


21

la Kiswahili Fasaha, 2010: 395). Hivyo, sauti hizo si sahihi kuzitumia tofauti katika Kiswahili kwani zinabadilisha maana iliyokusudiwa.

**Mofolojia**

Sarufi maumbo (mofolojia) ni taaluma inayohusisha uchambuzi wa maneno kwa kuchunguza jinsi maneno yalivyoundwa (Wasana-Chomi, 2013). Naye Rubanza (1996) anasema kwamba mofolojia ni utanzu mmojawapo katika tanzu za isimu unaoshughulikia vipashio vya lugha na mpangilio wake katika uundaji wa maneno. Vipashio hivyo vya lugha huitwa mofimu. Maneno katika lugha ya Kiswahili huundwa kwa vipengele vya usemi vidogo na vikubwa vinavyowekwa pamoja kwa kufuata utaratibu fulani maalumu. Vipande hivi, vinaweza vikawa vile vyenye kuundwa kwa kitamkwa kimoja tu au vile vyenye kuundwa kwa vitamkwa vingi. Vipande vya usemi katika lugha ya Kiswahili ni kama vifuatavyo katika mfano wa. 1:

*i. m, u, t, a*
*ii. ot-, ka-, ki-, tu-, ik-, pa-*
*iii. temb-, pungu-, chungu-*

Mfano 1 (i) hapo juu unaonesha sauti au kitamkwa kimojakimoja wakati 1 (ii) unaonesha vitakwa viwiliviwili na 1 (iii) unaonesha vitamkwa zaidi ya viwili. Vipande hivyo huweza kuwekwa pamoja kwa mpangilio maalumu kama huu ufuatao katika mfano wa 2 kwa ajili ya kuunda maneno katika Kiswahili. Maneno ambayo wazungumzaji wa lugha hii wanayatumia katika mawasiliano yao ya kila siku. Tuchunguze mfano wa 2:

*i. m-tu, u-tu,*
*ii. pat-a, o-ta, ka-a, ka-li-a, temb-e-a, pungu-a, chungu-a.*

Katika mfano huo wa 2 kuna vipande vya maneno ambavyo vinasimama kama viambishi awali na tamati na vingine ni vinasimama kama mzizi wa neno. Hivyo ni dhahiri kwamba katika mifano hiyo, kuna viambishi vinavyotangulia na vile vinavyofuata mizizi ya maneno. Viambishi vyote hivyo, vinawekwa kwa mpangilo maalumu unaokubalika katika isimu ya lugha yoyote ile. Hivyo, inapotokea utaratibu wa upachikwaji wa viambishi unapokiukwa, ndipo pale tunaposema kuna upotoshwaji wa kimofolojia katika lugha husika. Katika lugha viambishi vya maneno vinaweza kuwa katika hali ya umoja na wingi. Katika utafiti huu imebainika kwamba baadhi ya wanafunzi, wanafanya makosa ya kimofolojia bila wao wenyewe kujua. Mathalani data ifuatayo katika mfano wa 3 inadhihirisha hali hiyo.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| i. dhumuni | madhumuni |
| ii. dhehebu | madhehebu |
| iii. shaka | mashaka |
| iv. saa | masaa |
| v. muda | mida |
| vi. upungufu | mapungufu |

Tukichunguza kwa makini mifano iliyopo hapo juu, tunaoana kwamba, maneno haya ni maarufu sana tumeyazoea na tunayatumia mara nyingi katika mazungumzo yetu. Hata hivyo, pamoja na mazoea hayo baadhi ya wanafunzi wanayatumia kimakosa. Jambo hili, limejidhihirisha waziwazi katika utafiti huu. Kiukweli katika isimu ya lugha ya Kiswahili, maneno *madhumuni* na *madhehebu* hayana umbo la umoja yaani, kiasili maneno haya hayana viambishi vya umoja na badala yake yanakubali viambishi vya wingi tu. Hivyo maneno *dhumuni* na *dhehebu* si sahihi katika Kiswahili. Hii ni kinyume na matumizi ya maneno hayo kwa baadhi ya wanafunzi wa MNMA ambapo wanadhani


22

kwamba silabi *ma-* iliyopo mwanzoni mwa maneno hayo inaonesha wingi. Jambo ambalo sio sahihi katika isimu ya lugha ya Kiswahili sanifu, si kila neno linaloanza na *ma***-** ni kiambishi cha wingi.

Aidha, maneno *shaka, saa, muda* na *upungufu*, katika utaratibu wa isimu ya lugha ya Kiswahili, hayana umbo la wingi. Tukiwa na maana kwamba, umoja na wingi wa maneno hayo ni sawa tu. Vilevile, imebainiaka katika utafiti huu kwamba, wakati mwingine baadhi ya wanafunzi wanaosoma isimu ya Kiswahili wanalitumia neno saa kwa kuongeza silabi *li***-** wakidhani kuwa silabi hiyo, inawakilisha umoja wa neno *saa* hivyo, hulitamka kama *lisaa*. Katika isimu ya lugha ya Kiswahili si sahihi kutumia neno *lisaa.* Matatizo kama hayo, ni mengi na yameshazoeleka katika mazungumzo na hata katika maandishi ya kazi mbalimbali za kitaaluma wanazopewa wanafunzi darasani.

**Sintaksia**

Sintaksia ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake (Kihore na wenzie 2012). Kipengele hiki kinajikita zaidi katika kuchunguza sheria, kanuni na taratibu ambazo ni lazima zifuatwe katika kuyapanga maneno ya lugha husika katika mfuatano unaokubalika. Kila lugha ina upekee wake wa kuyapanga maneno katika sentensi. Kwa mantiki hiyo, kwa mujibu wa Massamba (2017) maneno ya lugha yoyote ile iwayo duniani kote hayakuvirigizwavirigizwa tu katika sentensi bali yamepangwa kwa mfumo kuntu unaofuatwa na wazawa wa lugha inayohusika. Endapo, mathalani, utaratibu huo utakiukwa, matokeo yake yatakuwa ni kutoa sentensi ambazo hazikubaliki kulingana na taratibu za lugha hiyo. Sanjari na hilo, sintaksia pia hushughulika na namna maneno yaliyomo katika sentensi za lugha husika yanavyohusiana. Hii ina maana kwamba sintaksia huchunguza ni mfuatano upi wa maneno unaokubalika katika lugha hizo. Kwa mfano, ni kategoria zipi zinazokubali au zisizokubali kufuatana au hata kuchunguza ni uendanaji upi wa kimantiki unakubalika au haukubaliki katika lugha hizo.

Makosa haya yanajitokeza kwa hali mbalimbali. Yanaweza kuwa ya kutumia miundo isiyokubalika, kuongeza viambishi kwenye maneno yanayojenga sentensi, kuacha baadhi ya maneno na pia masuala ya kiuakifishaji katika sentensi. Hebu tuchunguze mfano wa 4 ufuatao:

i. *Ningependa kukuona.*
ii. *Huwezi**jua**.*
iii. *Ninaomba **unijuze** yaliyotokea huko.*
iv. *Si **tu** hodari wa masomo bali na michezo vilevile.*
v. *Kulikuwa na**uvunjifu** wa amani.*
vi. ***Uwepo** wako ni muhimu.*
vii. *Namsubir**ia** hapa.*
viii. ***Kama haitoshi**.*
ix. *Vita **hii** ni kali sana.*
x. ***Rafiki** yake **na** Mwajuma.*
xi. *Mwanafunzi **kaa chini** usifute ubao.*
xii. *Rekebisha/kerebisha saa yako imepoteza majira.*
xiii. *Watu **kumi na nne wamepotea***

Sentensi hizo tumezikusanya kutoka kwa wanafunzi wanaosoma kozi mbalimbali za ismu ya Kiswahili. Tukizichunguza tutagundua kwamba si sahihi kwa mujibu wa taratibu za isimu ya Kiswahili. Tukianza na sentensi ya (i) Ni sentensi yenye muundo wa Kiingereza *(Iwould like to see you)*, Vilevile, Sentensi ya (iv) *Si **tu** hodari wa masomo bali na michezo vilevile* ya (vi) ***Uwepo** wako ni muhimu* na ya (viii) ***Kama haitoshi*** zimechukua muundo wa lugha ya Kiingereza na haziko katika muundo

wa asili wa lugha ya Kiswahili. Sentenzi ya (ii) lazima kitenzi kibebe kiambishi *ku-* kinachoonesha hali ya urejeshi hivyo, kitenzi sahihi huwezi *kujua***.** Katika sentensi ya (iii) kitenzi *unijuze* kimetumika kimakosa, kitenzi sahihi ni *unijuvye.* Vilevile, sentesi ya (v) kitenzi *uvunjifu* sio sahihi, kitenzi sahihi *ni* u*vunjaji* Katika sentensi ya (vii) Kitenzi *namsubiria* sio sahihi kinapaswa kuwa *namsubiri*. Katika sintaksia kitenzi *namsubiria* kinachanuza maana tofauti na iliyokusudiwa.

Katika sentensi ya (ix) neno *hii* sio sahihi katika sintaksia ya Kiswahili tunaseama *vita hivi ni vikali*. Sentensi ya (x) neno *rafiki* kwa maana ya mtu mnayeaminiana kwa kila jambo, linatumika zaidi kwa wanaume. Wanawake wanaoaminiana na kupendana neno sahihi katika lugha ya Kiswahili ni *shoga.* Shoga ni msamiati rasmi wa lugha ya Kiswahili na wala si matusi kama ambavyo baadhi ya wanafunzi wanadhani. Katika sentensi hiyohiyo kiunganishi *na* kimetumika kimakosa. Ama katika sentensi ya (xi**)** maneno *kaa chini* kama yalivyotumika katika sentensi hiyo sio sahihi, katika Kiswahili. Ni sahihi zaidi katika sentensi hiyo kusema kaa kitako. Kaa kitako ni kitendo cha kuweka matako juu ya kitu (Kamusi la Kiswahili Fasaha 2010: 135). Hii ina maana kwamba, kaa kitako ni kitendo cha kukaa juu ya kitu chochote iwe kiti, sofa au chini kabisa kutegemea na muktadha husika. Hivyo katika muktadha wa darasani, sentensi hiyo ilimtaka mwnafunzi akae juu ya kiti chake. Kinyume chake *kaa chini* maana yake ukae sehemu ambayo haina kitu chochote cha kukalia yaani chini.

Kupitia njia ya usaili tumebaini kwamba baadhi ya wanafunzi wanadhani kwamba maneno *kaa kitako* ni matusi na wala sio rasmi kutumika katika Kiswahili. Tulipoendelea kuwadadisi kwa nini wanadhani ni matusi, sababu yao kubwa ilikuwa ni matumizi ya neno *kitako* ambalo linatokana na *tako* neno ambalo ni tusi kwa kuwa ni miongoni mwa sehemu za siri katika mwili wa mwanadamu. Hivyo basi, matumizi ya maneno haya yanategemea zaidi muktadha ingawa baadhi ya watu wanayatumia katika muktadha wa aina moja. Kwa upande wa sentensi ya (xii) kupitia mbinu ya ushuhudiaji tumebaini kwamba wanafunzi wanafanya makosa katika kulitamka neno *rekebisha* na badala yake wanalitamka *kerebisha*. Vilevile, tumebaini maneno mengine ambayo wanafunzi wanashindwa kuyatofautisha kama vile *wakilisha/wasilisha*. Badala ya kutumia neno *wasilisha* baadhi ya wanafunzi wanatumia *wakilisha* au maneno *wamapochopocho/machopochopo* badala ya neno *mapochopocho* baadhi ya wanafunzi wanatumia *machopochopo*. Katika mifano kama hiyo tumebaini kuwa baadhi ya wanafunzi wanafanya makosa ya kimatamshi tu, kimaandishi hawafanyi makosa. Hali hiyo tumeibaini kupitia mbinu ya ushuhudiaji pamoja na hojaji walizozijaza. Hata hivyo kuna baaadhi ya wanafunzi wanafanya makosa ya kimatamshi pamoja na kimaandishi kwa kuwa wanayachanganya katika matumizi na kuyatumia vinginevyo.

Mwisho, katika sentensi ya (xiii) isemayo *watu kumi na nne wamepote*a imekosa upatanishi wa kisarufi wa maneno *watu kumi* na neno *nne.* Katika sintaksia ya Kiswahili kuna baadhi ya nambari ambazo lazima zibebe upatanishi wake wa nomino. Mathalani tunasema *watu kumi na wanne, kumi na watano, kumi na watatu* n.k. Hata hivyo, baadhi ya nambari zinakataa utaratibu huo kwa mfano hatuwezi kusema *watu kumi na wasita* au *kumi na wasaba.* Hii ni kwa sababu sintaksia ya Kiswahili inakataa utaratibu huo. Hivyo, makosa kama hayo yalibainika kwa wanafunzi wakati walipojaza hojaji pamoja na usaili. Baadhi yao walishindwa kutumia upatanishi unaofaa wa nomino na nambari. Kwa mfano walisema *watu kumi na nne* au *watu kumi na tano.* Hivyo, imebainika kwamba wakati mwingine wanafunzi wanayafanya makosa kama hayo katika Kiswahili bila wao wenyewe kujua.

**Semantiki**

Kwa ujumla semantiki kama taaluma inachunguza maana katika viwango vitatu ambavyo ni: kiwango cha leksia, kiwango cha tungo au sentensi na kiwango cha usemi au matini. Hivyo kila mmilisi wa lugha humuwezesha kutambua sentensi zenye maana sawa, sentensi zenye maana


24

kinzani, sentensi zenye maana jumuishi pamoja na sentensi zenye utata. Hii ina maana kwamba watu ambao sio wamilisi wa lugha, wanashindwa kuzitambua na kuzitofautisha sentensi hizo.

Katika kipengele hiki cha semantiki baadhi ya wanafunzi wanafanya makosa mengi yanayotokana na utata. Utata ambao zaidi unajitokeza katika kiwango cha neno (leksia). Utata wa kileksia ni ule ambao unatokana na matumizi ya neno kuwa na maana zaidi ya moja katika sentensi (Massamba, 2004). Tutazame mifano ifuatayo:

i. *Baba yangu amenunua* ***mbuzi***
ii. *Joshua ana* ***panga***
iii. *John ameleta* ***kima***
iv. *Mletee dada* ***kata***
v. ***Ziwa*** *lake ni kubwa mno.*

Tukichunguza mifano hiyo kuanzia (i) hadi (v) tunaona kuwa, kuna maneno katika sentensi hizo yamekolezwa wino. Maneno hayo yana maana zaidi ya moja ambapo maana hizo ndizo zinazosababisha utata. Katika mfano wa (i) neno *mbuzi* lina maana mbili: maana ya kwanza mnyama anayefugwa na maana ya pili neno hilo lina maana ya kifaa kinachotumiwa kwa ajili ya kukunia nazi. Mfano wa (ii) neno *panga* linaweza kuwa na maana mbalimbali kama vile ya kifaa kama kisu kikubwa kinachotumika kwa ajili ya kukatia, maana nyingine inaweza kuwa mzimu, aina ya samaki wa baharini na vilevile, kitendo cha kuishi katika nyumba au hoteli kwa malipo ya kila muda maalumu ambao wahusika hao wamekubaliana.

Aidha, katika sentensi ya (iii) neno *kima* lina maana ya aina ya mnyama anayeitwa kima au nyama ya kusaga. Katika sentensi ya (iv) neno lililokolezwa ni *kata* ambalo linaweza kuwa na maana ya kitambaa au majani yanayopetwa na kuwekwa kichwani au begani ili kuzuia mzigo usimuumize mbebaji. Vilevile, neno *kata* lina maana ya kifaa kinachotengenezwa kwa kifuu au kopo chenye mpini mrefu ambacho kinatumika kwa ajili ya kuchotea maji. Katika sentensi ya mwisho neno *ziwa* linaweza kuwa na maana ya eneo kubwa la maji baridi lililozungukwa na nchi kavu. Pia neno hilo lina maana ya kiungo cha binadamu kinachotoa maziwa kwa ajili ya kumnyonyesha mtoto mchanga (titi au chuchu).

Halikadhalika baadhi ya wanafunzi wa MNMA wanafanya makosa yanayotokana na utata wa kimuundo. Utata wa kimuundo ni ule ambao unajitokeza katika kiwango cha sentensi. Kwa mujibu wa Massamba (2004) utata wa kimuundo ni aina ya utata ambao unatokana na muundo wa sentensi yenyewe, ingawa kila moja ya maneno yaliyotumika katika sentensi hiyo hayana utata. Juma (2016) anadai kuwa utata wa aina hii unaweza kutokana na mambo kadhaa. Miongoni mwa mambo hayo ni mfuatano wa maneno, matumizi ya viwakilishi vimilikishi visivyobainifu, udondoshaji wa vipashio muhimu katika sentensi, matumizi ya leksimu mbili ambazo maana yake si bainifu na matumizi ya kauli ya utendeka.

Utata wa kimuundo unaotokana na mfuatano wa maneno ni ule unaoonesha jinsi maneno hayo yalivyopangiliwa katika sentensi. Tuchunguze mifano ifuatayo:

*(i) Tafadhali waite vijana na wazee kumi.*
*(ii) Fatma amechapwa fimbo mbili na Mwajuma*


25

Sentensi hizi zmebainika kuwa na utata wa kimuundo. Sentensi ya kwanza inaweza kuchanuza maana zifuatazo: Maana ya kwanza idadi ya vijana na wazee ni kumi na maana ya pili idadi ya vijana haijuilikani lakini wazee ni kumi. Aidha, katika sentensi ya pili maana ya kwanza Fatma amechapwa fimbo mbili na Mwajuma, maana ya pili Fatma na Mwajuma wote wamechapwa fimbo mbili.

Aidha, utata wa kimuundo unaweza kutokana na viwakilishi vimilikishi ambavyo vinarejelewa katika tungo mbalimbali bila ubainifu. Mathalani:

i. *Jarome alitaka kumtumia Mussa ujumbe, lakini* ***simu yake*** *ilizima ghafla.*
ii. *Maimuna anataka kuolewa na Omar, ila* ***wazazi wake*** *hawataki.*

Katika mifano ya sentensi ya (i) na ya (ii) tunaona jinsi viwakilishi vilivyosababisha utata wa kimuundo. Viwakilishi *yake* katika sentensi ya kwanza havieleweki waziwazi kwamba simu iliyozima ilikuwa ya *Jarome* au ya *Mussa*. Pia katika sentensi ya (ii) kiwakilishi *wake* kinatufanya tujiulize swali kwamba wazazi wa Maimuna au wa Omar ndio ambao hawataki wawili hao waoane?

Vilevile utata wa kimuundo unaweza kutokea kutokana na udondoshaji wa baadhi ya maneno katika sentensi. Kwa mfano:

*(i) Ali alimuona mwizi* ***kabla hajaruka*** *ukuta.*
*(ii) Dereva alimgonga mtoto* ***wakati akikimbia barabarani.***

Mifano iliyopo hapo juu, inadhihirisha utata unaotokana na udondoshaji wa maneno *mwizi* na *mtoto* katika sentensi hizo. Sentensi ya (i) neno *mwizi* linasababisha utata kwa kuwa limedondoshwa baina ya maneno *kabla* na *hajaruka*. Hivyo, tunashindwa kuelewa kwa yakini ni nani hasa ambaye hajaruka ukuta kati ya *Ali* na *mwizi.* Pia katika sentensi ya (ii) neno, *mtoto* limedondoshwa baina ya maneno *wakati* na *akikimbia barabarani*. Haieleweki kwamba ni *dereva* au *mtoto* aliyekimbia barabarani.

Utata mwingine wa kimuundo ni ule unaotokana na kauli za utendea katika sentensi. Kauli hizo mara nyingi zinasababisha sentensi kuwa na maana zaidi ya moja. Tuchunguze mifano ifuatayo:

*(i) Kaka alimjeng**ea** mama yetu nyumba.*
*(ii) Mtoto alimwandik**ia** baba barua.*

Katika sentensi hizo mbili tunabaini utata ambao umesababishwa na kauli ya utendea iliyojitokeza katika vitenzi *alimjengea* na *alimwandikia*. Viambishi *ea*- na *ia*- vina athari kubwa katika sentensi hizo. Katika sentensi ya (i) tunapata maana mbili ambazo ni: mosi kaka ni fundi hivyo *alimjengea mama yetu nyumba*. Pili, kaka amejenga nyumba kwa niaba ya mama yetu (alitoa fedha na kumpa fundi ili ajenge nyumba kwa ajili ya mama yetu kuishi). Halikadhalika, katika sentensi ya (ii) maana ya kwanza mtoto ndiye aliyeandika hiyo barua ya baba ambapo maana ya pili inaonesha kwamba mtoto aliandika barua kwa niaba ya baba (mwandishi alikuwa mtu mwingine sio mtoto)

Utata wa kimuundo katika sentensi unaweza kujumuishwa katika kipengele cha kisintaksia pale tunapoangalia muundo pekee. Hata hivyo, kimaana utata huo wa kimuundo unaweza kujumuishwa katika kipengele cha semantiki.


26

## Hitimisho na Mapendekezo

Makala haya yameelezea kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa kozi mbalimbali za isimu katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa MNMA. Imebainika katika utafiti huu kwamba, kuna makosa ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia pamoja na kisemantiki ambayo yanafanywa na wanafunzi hao. Makosa mengi yanayofanywa, katika ismu ya lugha ya Kiswahili yamegundulika kwamba, yanasababishwa na athari za lugha walizozizoea. Lugha mama za wanafunzi ndizo zilizowaathiri na kuwafanya washindwe kuzitofautisha na kuzitamka sauti za lugha ya Kiswahili kwa usahihi. Hivyo, walimu wa isimu ya lugha ya Kiswahili, wanatakiwa kufahamu mathalani, muundo wa kifonolojia wa lugha mama za wanafunzi ambazo zinaleta athari kubwa za kimatamshi. Hapa hatukusudii kwamba, mwalimu ajifunze lugha hizo la hasha, bali walau awe na uelewa wa mpangilio wa sauti zinazowatanza wanafunzi. Endapo walimu watakuwa na umahiri huo, hakutakuwa na kikwazo cha kuelewa chanzo na suluhu za athari hizo.

Hivyo walimu wanatakiwa kuyadhibiti makosa haya ili yasiendelee kutendeka katika lugha ya Kiswahili. Kazi kubwa ya mwalimu ni kuwasaidia wanafunzi na kuwafahamisha njia zilizo bora zaidi matahalani njia za uainishaji wa ngeli za nomino. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wataweza kuona na kubaini jinsi makundi mbalimbali ya maneno yanavyogawanywa katika ngeli zake. Bila shaka endapo walimu watachukuwa juhudi za makusudi za kuwarekebisha wanafunzi, kwa kiasi kikubwa makosa kama haya yanaweza kupungua katika lugha ya Kiswahili.

Jambo jingine la msingi ambalo walimu wanaweza kufanya, ni kuwapa mazoezi mengi ya kufanya ili kugundua makosa hayo na kuweza kuyarekebisha. Walimu wanatakiwa wachukue juhudi za makusudi na kuweka msisitizo ama wa kuyapunguza makosa kama haya au kuyaondoa kabisa yaani yasiwe yanajirudiarudia kwa wanafunzi na kuendelea kuichafua lugha ya Kiswahili.

## Marejeleo


Athman, R. M. (2015). *Athari za Lugha ya Kiswahili katika Lugha ya Kiyao*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuuu Huria cha Tanzania.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Oxford University Press.

Chomi, E. W. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili.* TUKI.

David, M. (2021). Upenyezaji na Ukubalifu wa Mkururo wa Konsonanti katika Fonolojia ya Kiswahili: Mifano katika Maneno Yaliyokopwa kutoka Kiingereza na Kiswahili. Katika *MULIKA. 40 (1),* 2-11.

Habwe, J. na wenzake. (2010). *Darubini ya Isimujamii kwa Shule na Vyuo.* Phoenix Publishers.

Idarus, A. S. (2005). Makosa Yanayofanywa Mara kwa Mara katika Matumizi ya Kiswahili. Katika *Semina za Kimataifa. (1)* 173-179).

James, C. (1980). *Constractive Analysis.* Longman.

Juma, H. K. (2016). Utata na Uvulivuli wa Kisemantiki katika Kiswahili. Katika *Jarida la JAHAZI. (1),* 36-46.

Juma, S. U. (2021). *Ulinganishi wa Kiisimu baina ya Kipemba na Kingazija*. Tasnifu ya PhD [Haijachapishwa]. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lado, R. (1957). *Linguistics Across Cultures.* OUP.

Massamba, D. P. B. na wenzake. (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu., (SAMAKISA)*: TUKI.

Massamba, D. P. B. na wenzake. (2004), *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Secondari na Vyuo:* TUKI.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* TUKI.

Massamba, D. P. B. (2017). *Historia ya Kiswahili. Mtazamo Mpya 100KK Hadi 2000BK*: Kiswahili Development Ltd.



27

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia; Kwa Sekondari, Vyuo Vikuu vya Kati na Vyuo Vikuu*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili.* TUKI.
Mbilinyi, G. (2018). *Kuathiriana kwa Vipengele vya Kifonolojia katika Lugha ya Kiwanji na Kiswahili*. Katika *Kiswahili*. *(81),* 97-106
Msanjila, Y. P. na Wenzake. (2011). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo*. TUKI.
Munyua, J. G. (2007). Isimu na Mwalimu wa Sarufi ya Kiswahili; Umuhimu wa Maarifa ya Kiisimu Darasani. Katika *CHAKAMA.* 67-73.
Otiende, A. M. (2013). Athari za Kimofofonolojia za Kiolusuba katika Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya MA [Haijachapishwa]. Chuo Kikuuu cha Nairobi.
Rubanza, Y. I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.


28